

Diwani ya Msikicho



Ariba Book Publishers

Copyright © 2017

All rights reserved by **Barack Wandera**

No part of this book may be reproduced or transmitted in any form or by any means, graphic, electronic, or mechanical including photocopying, recording, taping or by any information retrieval system, without permission in writing of the publisher.

Printed by:

Capvim International Limited

P. O. Box 3673 – 00200

Nairobi – Kenya

Tel: +254 728240931

Email: capvimlimited@gmail.com

ISBN: 978-1546694816

1546694811

First published 2017

Second edition 2019

Design and Layout by: Robert Mutugi

Edited by: Verah Omwocha

Published: Ariba Book Publishers

Yaliyomo

Ukurasa

| | |
|---------------------------|-------------------------------------|
| | 1 |
| CHIMBUKO LANGU | 2 |
| SHAHA MSIKICHO..... | 3 |
| UTUNZI 'IS MY LIFE' | 6 |
| TALANTA | 6 |
| AMBA | 7 |
| KISWAHILI..... | 8 |
| TUA..... | 9 |
| NIPE WASAA (RHUSA) | 10 |
| MSIKICHO | 11 |
| SHUJAA MIE | 11 |
| FIKIRA | 13 |
| HESABU | Error! Bookmark not defined. |
| MARADHI | Error! Bookmark not defined. |
| KEMIA..... | Error! Bookmark not defined. |
| JELA | Error! Bookmark not defined. |
| TAMU IMEZIDI TAMU..... | Error! Bookmark not defined. |
| BABU ZETU | Error! Bookmark not defined. |
| UDHALIMU | Error! Bookmark not defined. |

HAYATI USTADH WAMBALE..... **Error! Bookmark not defined.**
KESHO **Error! Bookmark not defined.**
WANDERA MSIKICHO..... **Error! Bookmark not defined.**
MOI **Error! Bookmark not defined.**
KWANGU KWATEKETE... **Error! Bookmark not defined.**
SISEMI NENO..... **Error! Bookmark not defined.**
MVUMILIVU **Error! Bookmark not defined.**
MIGINGO..... **Error! Bookmark not defined.**
HONGERA BUTULA..... **Error! Bookmark not defined.**
MAISHA **Error! Bookmark not defined.**
KIFARANGA **Error! Bookmark not defined.**
MTENDA HAKI **Error! Bookmark not defined.**
MWANA HARAMU **Error! Bookmark not defined.**
MKUFUNZI (JULIUS OCHIENG) **Error! Bookmark not defined.**
NISICHOJUA..... **Error! Bookmark not defined.**
JANGA LA UKIMWI **Error! Bookmark not defined.**
(shairi la 2)..... **Error! Bookmark not defined.**
HESHIMA **Error! Bookmark not defined.**
NAKATAA..... **Error! Bookmark not defined.**
NIMEACHA USHAIRI **Error! Bookmark not defined.**
MAGEUZI **Error! Bookmark not defined.**
MIGOMO..... **Error! Bookmark not defined.**

UKABILA **Error! Bookmark not defined.**
KENYA MPYA **Error! Bookmark not defined.**
WAKENYA..... **Error! Bookmark not defined.**
KIU **Error! Bookmark not defined.**
SIASA CHAFU **Error! Bookmark not defined.**
NDARAMA ZIBADILISHWE..... **Error! Bookmark not defined.**
UWEZO **Error! Bookmark not defined.**
YUPI? **Error! Bookmark not defined.**
YESU KRISTU..... **Error! Bookmark not defined.**
WANADAMU **Error! Bookmark not defined.**
JANA **Error! Bookmark not defined.**
ILAHU **Error! Bookmark not defined.**
WAHYU WANGU..... **Error! Bookmark not defined.**
USIKICHO **Error! Bookmark not defined.**
NILIVYOUNBWA **Error! Bookmark not defined.**
BIN NDUNI..... **Error! Bookmark not defined.**
MAPOKEZI **Error! Bookmark not defined.**
NAFSI BADILI **Error! Bookmark not defined.**
MHABU WANGU **Error! Bookmark not defined.**
MAPENZI YA PESA **Error! Bookmark not defined.**
JANIBU HAU (MAURICE WEKOLA) **Error! Bookmark not defined.**

MWANA WA MAMA **Error! Bookmark not defined.**
MPENZI..... **Error! Bookmark not defined.**
UFISI **Error! Bookmark not defined.**
UTOVU WA ZIADA..... **Error! Bookmark not defined.**
FAMILIA YETU..... **Error! Bookmark not defined.**
MWANAMKE..... **Error! Bookmark not defined.**
HAWAJAVYAWA WAREMBO **Error! Bookmark not defined.**
NOMIWA MOKAMI **Error! Bookmark not defined.**
HUA WANGU..... **Error! Bookmark not defined.**
MAVAZI **Error! Bookmark not defined.**
BBI **Error! Bookmark not defined.**
MASHUJAA **Error! Bookmark not defined.**
HONGERA SAINT JOSEPH'S **Error! Bookmark not defined.**
VIJULANGA WA KISASA **Error! Bookmark not defined.**
UJANA NI MOSHI..... **Error! Bookmark not defined.**
UFISADI AU USAFIDI..... **Error! Bookmark not defined.**
WENYE NGUVU **Error! Bookmark not defined.**
JAMBO BORA DUNIANI **Error! Bookmark not defined.**
MBUNGE NA MWANANCHI **Error! Bookmark not defined.**
VIJANA..... **Error! Bookmark not defined.**
ARSHI..... **Error! Bookmark not defined.**
OBAMA..... **Error! Bookmark not defined.**

KAMPENI **Error! Bookmark not defined.**
E - L - I - M - U..... **Error! Bookmark not defined.**
MAISHA YANGU **Error! Bookmark not defined.**
MATIANG'I **Error! Bookmark not defined.**
MWALIMU ODUORI WAMBALE.. **Error! Bookmark not defined.**
WATOTO WA MTAANI **Error! Bookmark not defined.**
FUNZA **Error! Bookmark not defined.**
CHUO KIKUU MASENO..... **Error! Bookmark not defined.**
UTOVU WA ELIMU **Error! Bookmark not defined.**
MUADHAMU MWALIMU **Error! Bookmark not defined.**
UFUKARA..... **Error! Bookmark not defined.**
DAUDI ONGARORA..... **Error! Bookmark not defined.**
KULA MAISHA NA ADABU **Error! Bookmark not defined.**
SHULE YA WASICHANA BUTERE.. **Error! Bookmark not defined.**
Uhakiki wa Mashairi..... **Error! Bookmark not defined.**
Asili ya Ushairi wa Kiswahili **Error! Bookmark not defined.**
I istilahi za kishairi **Error! Bookmark not defined.**
Bahari/mitindo ya mashairi **Error! Bookmark not defined.**

Utangulizi

Diwani ya Msikicho ni mkusanyiko adhimu wa Mashairi nduni ya Kiswahili ambayo yanaakisi hali halisi hapa Kenya. Mengi ya haya Mashairi nilayatunga ningali katika shule ya Upili ya Butula haswa katika kidato cha pili Magharibi nilikosomea.

Mbinu kadha wa kadha za umalenga kama vile ukawafi, pindu, sabilia na msuko zimetumika katika kuwasilisha hoja mbalimbali, mengi ya Mashairi haya yakiwa ya kimapokeo ilhali kuna machache yasiyofuata arudhi. Mbinu hizi zitamfaidi mwanafunzi wa ushairi katika kukuza ufahamu wake katika ushairi na Kiswahili. Maswala aina ainati nimeyashughulikia kwenye hii Diwani nayo ni maswala yaliyo na mvuto kwenye uhalisia wa Wakenya na Waafrika yakiwemo: uzalendo, sanaa, utu na uungu, mapenzi, ndoa na jamii, siasa, ujana na utendakazi, malimwengu na maswala ibuka, elimu na ulalahoi na mengineyo.

Mengi ya haya maswala ni kutokana na yale nimeyapitia maishani ambayo nimeyanakili ilhali mengine ni ya kubuni ambayo ninaazimia yalete mabadiliko katika jamii kama mojawapo ya vima vya ushairi kuelimisha jamii na kuonya wanajamii dhidi ya maovu, maonevu na utepetevu. *Msikicho* ina maana asiye na kicho yaani asiye mwoga, Jasiri. Limetokana na kuunganisha kiambishi *msi* pamoja na neno *kicho* ambacho ni kisawe cha hofu. Sababu haswa ya kuchagua kichwa hiki ni kuwa kila jambo maishani linahitaji ujasiri, yakiwemo mengi ambayo mie binafsi nmefanikiwa kuyafanya ambayo yametokana na kuuvua woga na kuvalia ujasiri.

Lugha ya Kiswahili ni tunu ambayo Mola aliiruzuku bara la Afrika. Licha ya kusomea lugha za kigeni kama vile

Kiingereza naliona vema kuandika Diwani hii katika lugha yetu tukufu ya Kiswahili, ili kukikuzi na pia kutoa ile dhana potovu hapa Kenya vile watangulizi wangu kama Ken Walibora, Wallah Bin Wallah na wengineo walianzisha. Kwamba lugha hii si ya wanamwambao pekee bali yetu sote hapa nchini Kenya na Afrika kwa jumla.

Kiswahili kinalandana na lugha nyinginezo za Kiafrika hasa za Kibantu kama vile Kiluhya, Kikikuyu, Kigusii, Kisukuma, Kiganda, Kizulu, Kiswazi, Kishona, Kiyoruba, Kiigbo na Kilingala. Pia kuna mtagusano kati ya Kiswahili na lugha za Kigeni kama vile Kiarabu jambo ambalo linafanya lugha hii iwe rahisi kujifunza kwa wanabara wanaozungumza Kiarabu kama vile Misri, Sudan, Tunisia na Morocco. Kwa kifupi lugha hii ni rasilimali muhimu iwapo tu wanabara watakubali kuikumbatia kikamilifu.

Ama kwa kweli lenye mwanzo halikosi mwisho. Jamvi nalikunja katika kuwaheshimu wale walionikuza na kuniauni katika huu ulingo. Ni wengi, ila nimewataja wachache:

Tabaruku

Wazazi wangu Richard Oduor Okuba na Tata Nasio Nafula walionipa malezi bora na mapenzi pamoja na kunitia moyo katika utunzi.

Pamoja na:

Jamaa na marafiki kwa jumla, **PAWA254, MUELISA, *Department of Literary studies, Department of Linguistics,*** Ndugu Conrad Muyoti wa West FM, Mchungaji Obongita kwa niaba ya **K.A.G-Maseno**, Bi Queen Simiyu wa shule ya msingi kule Khaoya kwa niaba ya walimu wangu wa shule ya msingi.

Bw Julius Oching wa Butula kwa niaba ya walimu wangu wa sekondari, Profesa Florence Indede wa Idara ya Kiswahili na lugha nyingine za Kiafrika, Profesa Edwards Kochung Mlezi wa MUES na Dean *School of Education* kwa niaba ya wahadhiri wangu kule Maseno University na Jamii ya Butere Girls ikiongozwa na Mwalimu Mkuu, Bi Jenipher Omondi.

Barack Wandera Mwana W'Oduori

Maseno University, Mei 2019

I. TUNGO ZA KUTUKUZA SANAA

Inayo vima Sanaa

Mashairi yanafaa

Kwa jamii na jamaa

Tuupatapo wasaa

Wasia unatujaa

Mwangata kama wa taa

Unaotuelekeza

CHIMBUKO LANGU

Maswali nimeulizwa, kuhusu wangu uzawa
Wao wataka kujuwa, wapate jibu muruwa
Wanataka kutambuwa, chanzo cha huu upawa
Nanadi chimbuko langu

Wengi waeleza kuwa, ni mzaliwa wa pwani
Jinsi ninavyodhaniwa, ni mwenyeji wa Diani
Na wengine waelewa, ni mwisilamu kidini
Nanadi chimbuko langu

Mimi siye wa wangozi, wala wa kule Dodoma
Bali mimi ni mkazi, na mwenyeji wa Bungoma
Na huu wangu utuzi, ni hujazi ya Karama
Nataja chimbuko langu

Umashuri ni utuzi, wa nudhumu na ujuzi
Waghani wa siku hizi, na watunzi chipukizi
Msifanye uchafuzi, ambao haupendezi
Naamba chimbuko langu

Mwalimu wa kimsingi, alinikuza upawa
Yeye kanifunza mangi, vitabu kuvichambuwa
Mwalimu hakunikengi, nilipata kukolewa
Nataja chimbuko langu.

Kiswahili ni atia, Maulana katupea
Ni nujumu kujitia, bahati kuipokea
Lengo tutaafikia, Kiswahili kugobea
Nataja chimbuko langu

SHAHA MSIKICHO

Katika karne hino, kama ninavyotambuwa, Msikicho ndiye shakha
Mashairi mengi mno, barmamba alotowa, yalojawa na nasaha
Kweli hanao mfano, mtunzi alokolewa, yeye aliye na jaha
Ana fufuri maono, kijana aliyejawa, na magwadu yenye siha
Tangu darasa la tano, Msikicho alikuwa, malenga mwenye staha
Anazifahamu ngano, pia za lugha saluwa, wa Kiswahili msheha
Yeye ni kama ndoano, ndoano inayovuwa, watu kwa lugha fasaha
Aendapo kongamano, la malenga kuchaguwa, huwatinga kwa buraha
Hashindi kwa vurugano, tena sio kwa uluwa, ndiposa akawabwaha
Yeye ni kama tabano, tabano yake Jalawa, dunyani kuleta raha
Tena ni kama maneno, maneno kwake mgonjwa, ya kuondoa karaha
Mnishike kwa mikono, wasomi kunielewa, nisipatwe na jaraha

Muadhamu Msikicho, mtunzi alo mahiri
Muadhamu Msikicho, mshairi mashuhuri
Muadhamu Msikicho, ya karne hii johari
Muadhamu Msikicho, rekodi za yalojiri
Muadhamu Msikicho, wa uswahili fahari
Muadhamu Msikicho, mwangata wa mafakiri
Muadhamu Msikicho, mrithi wa ushairi
Muadhamu Msikicho, malenga wa lugha nzuri
Muadhamu Msikicho, kijana mwenye nadhiri
Muadhamu Msikicho, anotunga kwa kadiri
Muadhamu Msikicho, mpawa wake *Qahari`*

Atawala ushairi, barani hadi bahari
Barani hadi bahari, akapate kunawiri
Akapate kunawiri, bila hata ya dosari
Bila hata ya dosari, ndipo aitwe hodari
Ndipo aitwe hodari, mtunzi alo jasiri
Mtunzi alo jasiri, alojawa na basuri

Alojawa na basuri, ajua kunga fufuri
Ajua kunga fufuri, na misemo furifuri
Na misemo furifuri, na tarekhe zilojiri
Na tarekhe zilojiri, tarehe za ushairi

Huyu shakha alizawa, hapa Bungoma mjini
Naye katu hajajawa, nazo kasumba za Pwani
Wale wanaomjuwa, wanaweza kukirini
Kwamba yeye ni mzawa, na mkazi wa barani
Msikicho twatambuwa, ndiye malenga nduuni
Na weledi a'lelewa, kishaye kuhimizweni
Na wale wanoelewa, wanoelewa kanuni
Wanadai ana mbawa, mbawa zisizo kifani
Na wengi wamependezwa, na tungo zake thamani

Alipata nyota ile, *Bar*
Kutoka kwa mteule, Mola
Akawaiga wakale, Hajji
Walotunga misemele, Guru
Na yule alomvyale, Mama
Pamoja na mzele, Baba
Ndiposa akafikile, Shakha
Chao wakale kilele

Si mtunzi wa kikale maizi
Ni shakha atungaye sikuhihi
Afwata nyayo za watangulizi
Semi za lugha mbovu hapachizi
Kuboronga Kiswahili hawezi
Tungoze zitafaidi vizazi

Msikicho ana ndoto, ya kukuza Kiswahili
Na kuondoa magezo, yakuwa ni lugha finyu
Mabuku atayaunda, Mola ampe uhai
Kama ya shekisifia, mtunzi wa Wingereza
Ana azimia kuwa, shesifia mswahili
Kiswahili kitukuzwe, vizazi hadi vizazi

Kwa vijana wanoezi, lugha yetu ya taifa
Mzidishe matumizi, na kuipatia sifa
Sheng' hawazungumzi, wasotaka lugha kufa
Kwani lugha ya shengazi, kwa Kiswahili ni bafa
Basi sheng' tuzime zi, kuyaondoa maafa

Baba mama na watoli
Wasopenda Kiswahili
Madharau sikubali
Lugha yangu itukuzwe

Wandera Msikicho
Mtunzi aso na kicho
Amekuja kwa vificho

Na mwenyezi Mungu, Moola
Nilipendwa tangu, azala

Ndiposa kanitunuku, talanta hino azizi, Kiswahili nikikuze vizuri

UTUNZI ‘IS MY LIFE’

Japo Mariga kasema, soka ndo maisha yake
Mie hapa naposoma, hadi mbingu niifike
Utunzi utanivama, upawa unifunike
Utunzi ‘is my life!’

Nitatunga mashuara, na tungo nyingine nyingi
Wakale nitawahara, utunzi haunitingi
Najua ipo tijara, pengine mie silengi
Utunzi ‘is my life!’

Fasihi kuichambuwa, ndio langu kusudio
Kwani sasa natambuwa, ya kwangu matarajio
Ninafurahi nikiwa, chanisela wa Ohio
Utunzi ‘is my life!’

TALANTA

Talanta hino azizi, Mola aliniruzuku
Drama ‘meshika mizizi, ‘mepunguza ukasuku
Naiga bila ‘kuseaze’, mchana pamwe usiku
Ama kwa kweli talanta, yarekebisha mienendo

Hapo awali n’likuwa, mtundu alotajika
Madili kengeukiwa, shetani nikaibuka
Jina baya nikapewa, walimu *wakaboeka*
Ama kwa kweli talanta, yarekebisha mienendo

Vileo navyo nkanywa, anasa ikaniniteka
Mihadarati n’kalewa, mawaidha n’kaepuka
Uzinzi nkazidiwa, Staa nikasifika
Ama kwa kweli talanta, yarekebisha mienendo

Wasia nikaupata, mui n'kageuka mwema
Nikaiondoa nta, jukwaani *n'katetema*
Nikaikuza talanta, n'kaigiza ja Mutuma
Ama kwa kweli talanta, yarekebisha mienendo

Tatizo langu la karo, talanta ikafadhili
“Tumwauni huyu Vero, anayo mema madili
Kaudondosha utoro, na mwenendo kabadili”
Ama kwa kweli talanta, yarekebisha mienendo

AMBA

Amba

Tamba

Kwamba

Kuloloma lumba

Sio kuimba Rhumba

Pia ufahamu kuimba

Nyimbo kama vile samba

Pamoja nako kujipamba

Kujipamba sambamba

Hakubambi

Jamba

KISWAHILI

Tarekhe za Kiswahili, Kiswahili cha Wangozi
Washungwaya wa Somali, Wasomalia wakazi
Waswahili wa azali, Waswahili tangulizi
Wasomi tumeamua, Kiswahili tutukuze

Jambo lililowauni, ni roho ya ukarimu
Kuwakaribisha weni, kwa bashasha kemkemu
Haswa wa Uarabuni, na ajmina wa humu
Wasomi tumeamua, Kiswahili tutukuze

Hamna sehemu tata, ilo kaika shairi
Maswali ukiyapata, utafanya bila shari
Na mitihani kupita, utaipita kwa cheri
Wasomi tumeamua, Kiswahili tutukuze

Vijana wa sikuhizi, waswahili chipukizi
Tumeamua kuenzi, lugha katika kizazi
Kuipatia makuzi, makuzi yalo azizi
Wasomi tumeamua, Kiswahili tutukuze

Wasomi walo shuleni, hata pia wa vyuoni
Kiswahili msihini, shuleni hata nyumbani
Kishaye muiamini, lugha aula barani
Wasomi tumeamua, Kiswahili tutukuze

Mwisho hapa nimefika, mdomoni kufungika
Wasomi tunavyotaka, Kiswahili kutukuka
Na siyo kudimika, kama inavyodaika
Wasomi tumeamua, Kiswahili tutukuze

TUA
Tuwa
Najuwa
Natambuwa
Eti ya kuwa
Si kwa ubinguwa
Wala si kwa uluwa
Wapata kufanikiwa
Au hata kubarikiwa
Ni jaha – sudi maridhawa
Elakini kwa kuwa mpendwa
Simaanishi kuwa hutapingwa
‘Na maana utaisha kama maua
Ni maisha yaliyo ya kufurahiwa.

NIPE WASAA (RHUSA)

Nafusi yangu nafusi, naomba unipe rhusa
Rhusa ya kutia kasi, na kujipiga msasa
Rhusa iwayo asasi, inayoleta hamasa
Ruhusa ya ufanisi, “La hashu” kunitikisa
Nafusi yangu siasi, ‘Ustawi’ nakuasa
Naomba nipewe rhusa, nipate mafanikio

Mie hapa gombe dume, naomba nipewe tiba
Nina ari toka lime, munitie kwa zeriba
Ninatokea mahame, japokuwa nina heba
Kule kwenye nchi kame, kuliko na maji haba
Naomba nipewe rhusa, nipate mafanikio

Japo wengi tauliza, kwanini yuaja huku
Haya mie nakujiza, nina haja ya kupiku
Kisha wapate nituza, inakuja hii siku
Naomba nipewe rhusa, nipate mafanikio

Iwapo hujaelewa, haya ninayosema
Nina maana yakuwa, shule ile nimehama
Naomba nipewe rhusa, nipate mafanikio

Wazazi wangu naomba, munipe huu wasaa
Naomba nipewe rhusa, nipate mafanikio

Walimu wangu shuleni, shule mpya nakoenda
Pamoja tusimameni, ufanisi kunitanda
Naomba nipewe rhusa, nipate mafanikio

Wanafunzi wenzi wangu, umoja tuutumie
Nayo makuu majungu daima tuyasikie
Halafu tumwombe Mungu, Mola atusaidie
Naomba nipewe rhusa, nipate mafanikio

MSIKICHO

Msikicho
Usiye na kicho
Fungua yako macho
Kisha upokee kocho
Usichukue kisicho
Hicho
Kilicho
Kochokocho

SHUJAA MIE

Mie shujaa Wandera, shujaa wa karne hino
Watunzi nimewahara, wakenya na wa Ureno
Bungoma hadi Harara, hamna wangu mfano
Wandera ni shujaa!

Vita ninavyopigana, sio vita vya mikuki
Ni vita vya kupeana, tungo na kuzihakiki
Mabongo ndo ya maana, bilazo mbali sifiki
Wandera ni shujaa!

Mbio pia nakimbia, uga ule kitabuni
Na nchi kuitwalia, medali za *goldeni*
Hakuna nilosikia, kaniita bustani
Wandera ni shujaa!

Japo bado mwanafunzi, tungo nyingi nimeunda
Tungo hizo za utunzi, na tungo zenye kufunda
Kiswahili nakienzi, mizizi nimeipanda
Wandera ni shujaa!

Mpiga mbizi marufu, kidimbwini ushairi
Tena mie sina hofu, kupinzana na jabari
Yule mnayemsifu, kama ustadhi Guri
Wandera ni shujaa!

Tumkumbuke Baraki, kama angali mzima
Ufisadi hautaki, hili haachi kusema
Wakenya hatupikiki, chungu moja na lukuma
Wandera ni shujaa!

Hata kama ni mchanga, mwanasoka Msikicho
Mabao anayatinga, wavuni bila ya kicho
Anazifahamu chenga, za shairi kochokocho
Wandera ni shujaa!

Mnojiona mabingwa, mie kwenu limbukeni
Yale ninayoyajuwa, mlifahamu zamani
Basi swali nalozuwa, tungo ngapi mtungeni?
Wandera ni shujaa!

FIKIRA

Fikira yangu shukura
Kunongoza kwa busara
Maisha nikayahara
Kongole fikira zangu.

Ungekuwa mui hasa
Ningekumbwa na mikasa
Na maisha kuyakosa
Kongole fikira zangu.

Mishipi uliikaza
Watu waliponitwaza
Na nafsi kuikuza
Kongole fikira zangu.

Jambo jingine sikiza
Lile linofurahiza
Kunilinda uliweza
Kongole fikira zangu.

Shida ziliponitanda
Hukuniacha kudunda
Kwenye lindi la kidonda
Kongole fikira zangu.

Mwisho fikira nasema
Usiwe kama mgema
Wateja anaawatema
Kongole fikira zangu